

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZAMITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA
(Barua zote ziadikwe kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya)

Simu:
Nukushi:
Tovuti: www.buchosadc@go.tz



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji
(W)
S.L.P. 44
Buchosa
SENGEREMA

Kumb.Na.AB.74/211/01


14/05/2018

YAH: KUITWA KWENYE USAILI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa, anapenda kuwatangazia waombaji wa kazi ya Mtendaji wa kijiji daraja la III kuwa, usaili kwa waombaji waliokidhi vigezo, utafanyika kuanzia tarehe 21/05/2018 na 22/05/2018 saa 3:00 asubuhi, katika ukumbi wa kanisa la AICT Nyehunge uliopo makao makuu ya Halmashauri ya Buchosa.

Wasailiwa wanatakiwa kuzingatia yafuatayo:-

1. Kila msailiwa anatakiwa kufika na Vyeti halisi (origina certificates) vya kidato cha nne, taaluma. Na Cheti halisi cha kuzaliwa. "Provisional results, testimonials, result slips" hazitakubalika.
2. Kila msailiwa anatakiwa kufika na kitambulisho kwa ajili ya utambuizi kati ya vifuatavyo:- kitambulisho cha mpiga kura, kitambulisho cha uraia,, leseni ya udereva, hati ya kusafiria na kitambulisho cha bima ya afya.
3. Wasailiwa waliosoma nje wanatakiwa wahakikishe vyeti vyao vimehahakikiwa na mamlaka husika
4. Kila msailiwa atajiharimia nauli, chakula na malazi.
5. Wasailiwa wanatakiwa kuzingatia muda.
6. Usaili wa maandishi utafanyika tarehe 21/05/2018 na kwa wale watakaofuzu watafanya usaili wa mahojiano tarehe 22/05/2018
7. Waombaji ambao majina yao hayakuorodheshwa wahesabu kuwa maombi yao yamekosa sifa na hivyo wasifike kwenye usaili huu.


Joyce P. Manyanda
KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W),
BUCHOSA

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUCHOSA

Nakala: Mbao zote za matangazo.
Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Buchosa